JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

**KATIKA KAMATI YA MAUDHUI YA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA, DAR-ES-SALAAM**

**SHAURI NA. 13 – 2021/2022**

**DHIDI YA**

**DARMPYA ONLINE TV**

**UAMUZI**

**UAMUZI WA KAMATI YA MAUDHUI KUHUSU MASHTAKA YA UKIUKAJI WA KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA (MAUDHUI YA UTANGAZAJI MTANDAONI), 2020.**

## 1.0 MAELEZO KUHUSU UKIUKAJI WA KANUNI

1.1 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ilitoa leseni kwa kampuni ya **PAMOJA BUILDING MATERIALS LIMITED** kwa ajili ya kuchapisha na kutangaza habari mbali mbali mtandaoni kwa kupitia vituo vyake vya utangazaji vya **DARMPYA ONLINE TV** na **DARMPYA BLOG**.

1.2 Kwa mujibu wa Kanuni ya 19 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji Mtandaoni), 2020. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ina jukumu la kusajili na kusimamia watoa huduma wote wa maudhui mtandaoni ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua stahiki za kisheria dhidi ya mtoa huduma ye yote atakayekiuka Kanuni za Maudhui Mtandaoni au Sheria nyingine.

1.3 Mnamo tarehe 17 Juni 2022, Kituo cha **DARMPYA ONLINE TV** kilituhumiwa kukiuka kanuni za utangazaji kwa kutoa taarifa za upotoshaji, uchochezi na zisizokuwa na uthibitisho kwa lengo la kuupotosha umma kuhusu yanayoendelea Loliondo. Kwa mujibu wa Sheria na

taratibu zinazotumika kushughulikia mashauri ya kimaudhui, malalamiko yaliwasilishwa kwa Kamati ya Maudhui ("Kamati") kwa ajili ya kufanyiwa tathmini na tarehe 27 Juni, 2022 uongozi wa Kituo cha **DARMPYA ONLINE TV** ulitakiwa kufika mbele ya Kamati kwa ajili ya kutoa maelezo yake ya utetetezi wao dhidi ya tuhuma hizo.

## 2.0 KANUNI ZILIZOKIUKWA

2.1 Kwa kitendo cha kuutangazia umma taarifa zinazopotosha, za uchochezi, uchonganishi na zisizo na uthibitisho ambazo hazikutolewa ufafanuzi, **DARMPYA ONLINE TELEVISION** inatuhumiwa kukiuka Kanuni Na. 9(a),12(a)(i) na 16(1) pamoja na Aya ya 3 (a), (d),(g),(h) na (k) ya Jedwali la Tatu katika Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji Mtandaoni) 2020 kama ilivyofanyiwa marekebisho na Marekebisho ya Kanuni za Maudhui Mtandaoni za 2022, ambazo zinasomeka kama ifuatavyo:

*9. A licensee shall comply with all the terms and conditions of the licence and observe the following:*
*(a) ensure that online content is safe, secure and does not contravene the provisions of any written law;*

12. An Online Content Services License Category A shall be required to comply with the following conditions-
(a) in the case of online content service licensee, shall-
(i) adhere to journalism ethics and professional requirements as per the Media Services Act;

*16.-(1) A person shall not publish any prohibited content as set out in the Third Schedule*
*3. Public Security, Violence and National Safety*

*(a) content against the State and public order including content that aims to or publishes information, news, statements or rumors for the purpose of ridicule, abuse or harming the reputation, prestige or status of the United Republic, the flag of the United Republic, the national anthem or the United Republic's symbol, national anthem or its logos;*

*(d) content that would threaten the security of the United Republic or affect public order;*

*(g) content that incites, encourages or enables the commission of a crime against the United Republic or its citizens;*

*(h) content that is likely to threaten the stability of the United Republic or its safety, unity or security, or harming national unity or social peace;*

*(k) content that causes annoyance, threatens harm or evil, encourages or incites crime or leads to public disorder or that may threaten national security or public health and safety;*

## 3.0 WITO WA KUTOA MAELEZO YA UTETEZI.

3.1 Tarehe 21 Juni 2022, Kamati ya Maudhui ilikiandikia Kituo cha **DARMPYA ONLINE TV** wito wa kuwasilisha utetezi wa maandishi na kufika mbele ya Kamati ya Maudhui, tarehe 27 Juni 2022 saa 04:00 asubuhi kutoa utetezi wa mdomo dhidi ya tuhuma zinazowakabili.

3.2 Tarehe 27 Juni 2022, **DARMPYA ONLINE TV** iliwasilisha utetezi wake wa maandishi, Mkurugenzi. Pia, **DARMPYA ONLINE TV** ilifika mbele ya Kamati kutoa utetezi wao wa mdomo ikiwakilishwa na Wakili Msomi **Mpare MPoki**, Mkurugenzi wa DARMPYA ONLINE TV, **John Marwa,** "

## 4.0 KUSOMEWA MASHTAKA, KUSIKILIZA NA KUANGALIA MAUDHUI YA DARMPYA ONLINE TV YANAYOTUHUMIWA.

4.1 Kamati ya Maudhui iliisomea **DARMPYA ONLINE TV** mashtaka yake na pamoja na kuangalia maudhui yaliyochapishwa na **DAR MPYA BLOG.**

## 5.0 UTETEZI WA DARMPYA ONLINE TV

5.1 Katika utetezi wao wa maandishi, **DARMPYA ONLINE TV** walieleza kuwa baada ya kupokea wito wa Kamati, Uongozi wa Darmpya Online TV uliitikia wito wa kufika na kutoa maelezo ya utetezi wao mbele ya Kamati ya Maudhui. Utetezi wao ni kama ifuatavyo:

a) Kwamba, DarMpya Online TV, sio mmiliki wa ukurasa wa *twitter* unaotuhumiwa kufanya hilo kosa isipokuwa majibu /utetezi ulioletwa ni kwa sababu ya wito na sio kwamba tunakiri kuwa ukurasa huo una uhusiano wowote na DarMpya online TV.

b) Kwamba, kwa vile ni swala la kisheria kuwa ni lazima adhabu na hatua za kisheria zielekezwe kwa mmiliki au mwenye uhusiano na kosa, ni kweli kabisa na kwa ushahidi kuwa DarMpya Online Tv sio mmiliki wa ukurasa huo.

c) Kwamba, tunapinga vikali tuhuma hizi, kuwa hakukuwa na chapisho la maudhui yenye kupotosha umma, kuchochea na kuhatayarisha usalama wa nchi.

d) Kwamba, hakuna upotoshaji wa chochote katika habari iliyochapishwa wala taarifa ya uchonganishi na uchochezi kama barua yako (Kamati) inavyoeleza.

e) Kwamba, chombo chetu hakina madhumuni wala malengo ya kuchapisha maudhui ya kupotosha umma wala jamii badala yake kipo kwa ajili ya kufanya kazi ya kutoa taarifa kulingana na sheria za nchi pamoja na katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hasa ibara ya 18 ya Katiba, Sheria za Huduma ya Habari ya mwaka 2016, pamoja na sheria zinazoongoza vyombo vya habari mtandaoni kama Kanuni ya maudhui ya mtandaoni.

f) Kwamba, DarMpya Online TV haihusiki kwa namna yeyote ya ukurasa wa Twitter unaotajwa.

g) Kwamba, mwandishi wetu ndiye aliyenyang'wanya simu ili asirekodi na hivyo taarifa hiyo imechapishwa kulingana na maudhui yale yalitolewa na muhusika wa taarifa hizo, hivyo taarifa hiyo ni ya ukweli na mwandishi alikuwa eneo la tukio.

h) Kwamba, tunaomba Kamati ipitie kwa kina ushahidi uliopo na kujiridhisha iwapo Dar Mpya Online Tv imeweka chapisho hilo.

## 6.0 TATHMINI YA KAMATI

6.1 Kamati ya Maudhui imezingatia maelezo yote ya **Darmpya Online TV** na kubaini kuwa ukiukwaji wa Kanuni za Maudhui Mtandaoni kama ulivyobainishwa katika sehemu ya pili hapo juu ulifanywa na **DARMPYA BLOG** na sio **DARMPYA ONLINE TV**, ambao walipelekewa mashtaka na kuitwa mbele ya Kamati.

6.2 Pia, Kamati imegundua kwamba leseni za **DAMPYA ONLINE TV** na **DARMPYA BLOG** zilitolewa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania mwaka 2018 na kuisha muda wake mwaka 2021. Mpaka sasa, leseni hizo hazijahuishwa tena.

**7.0 MAELEKEZO YA KAMATI KWA DARMPYA ONLINE TV**

Kutokana yaliyobainika, Kamati inaielekeza **DARMPYA ONLINE TV** kuhuisha leseni zao za utoaji wa maudhui mtandaoni haraka iwezekanavyo kwa mujibu wa Kanuni za Maudhui Mtandaoni za 2022 kwani kuendelea kutoa maudhui hayo pasipo kuwa na leseni halali ni kinyume cha Sheria.

**8.0 UAMUZI WA KAMATI**

Baada ya kusikiliza utetezi wa Darmpya Online TV na kwa vile Kamati ya Maudhui kisheria inashughulika na mashauri yanayohusu ukiukwaji wa Sheria, Kanuni na Maadili ya Habari na Utangazaji kwa watoa huduma za utangazaji wenye leseni halali ya Mamlaka ya Mawasiliano, Tanzania, Kamati ya Maudhui imeamua kama ifuatavyo:

Inafuta mashtaka dhidi ya Darmpya Online TV kwa sababu zilizoainishwa katika tathmini ya Kamati katika 6.0 hapo juu na kwa mujibu wa Kifungu cha 44(2)(a) cha Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (Sura ya 172);

Uamuzi huu umetolewa Dar es Salaam leo tarehe **14 Julai, 2022.**

Haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu kwenye Baraza la Ushindani wa Haki Kibiashara (Fair Competition Tribunal – FCT) iko wazi ndani ya siku 21 (ishirini na moja) kuanzia siku ya kutolewa kwa uamuzi huu.

**Uamuzi huu umesainiwa na:**

**Ndalahwa Habbi Gunze**

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
20 BARABARA YA SAM NUJOMA
S. L. P. 474
14414 DAR ES SALAAM
TANZANIA

..................................................

**Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui**

**PAMOJA NA WAJUMBE WAFUATAO WA KAMATI YA MAUDHUI:**

1. **Derek Kaitira Murusuri** ..................................

2. **Jacob Gregory Tesha** ..................................